



Mifugo wenye afya



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Wanjohi J.M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-MUGUGA NORTH

S.L.P. 32, kikuyu


Simu: 0202700256

Baruapepe: vrckari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 38 /2008

Shilingi 20 za Kenya

**Wachanje mifugo dhidi
ya homa ya pwani ya
mashariki (ECF)**



Homa ya Pwani ya Mashariki (ECF) ni nini?

Huu ni ugonjwa unaopatikana katika nchi zilizoko upande wa Mashariki ya Afrika pekee na hua mifugo wapatao 120,000 wa umri wowote kila mwaka nchini Kenya.

Unasababishwa na wadudu walio sawa na wale wanaosababisha malaria kwa binadamu. Wadudu hao huambukizwa miongoni mwa wanyama kupitia kwa kupe wa hudhurungi (hushikilia karibu masikioni mwa wanyama).




Kupe wa hudhurungi wa sikio

Dalili ya mnyama aliyeambukizwa ugonjwa (ECF)

- Uvimbe wa koo-ni (ngaai)
- Tatizo na kupumua haraka

- Kula chakula kidogo (kupoteza hamu)
- Joto kuzidi (zaidi ya nyuzi 39.50°C)
- Maziwa kupungua sana (kwa ng'ombe anayekamuliwa)



Uvimbe wa koo-ni

Ugonjwa unadhibitiwa katika mahabara na daktari wa mifugo. Unaweza kutibiwa lakini kutambua mapema ni muhimu ili kuwe na mafanikio.

Jinsi ya kudhibiti na kutibu ugonjwa huu

- Kuwadhibiti kupe kwa kutumia dawa ya *acaricide* kwenye vidimbwi vya mifugo, kuoga mikono au kuwamwagilia.
- Kuwatibu mifugo wagonjwa.
- Kuwachanja dhidi ya ugonjwa.

Kuchanja dhidi ya ECF ni nini?

- Ni kuwadunga sindano inayosababisha ugonjwa huo na kutibu papo hapo. Mtindo huu unarejelewa kama kuambukiza na kutibu (KK).
- Mtindo huu wa KK unategemea ukweli kwamba mwili wa mnyama aliyeambukizwa na kupona huimarisha nguvu asili za kutoambukizwa tena akiwa maeneo yayo hayo.
- Badala ya kusubiri kuambukizwa kwa kawaida, kuchanja huko kunafanywa katika hali iliyodhibitiwa.
- KK huhitaji kufuatiliwa na mhudumu kutathmini matokeo.

Kuna faida zipi za kuchanja?

- Kupunguza vifo vya mifugo.
- Kipindi kirefu cha uwezo wa kiasili kutoka kwa chanjo moja.
- Kupunguza mtindo wa kupulizia dawa kutoka mara moja kila juma hadi mara moja kati ya majuma mawili au matatu.